# MOYO WA MUTU



**COPYRIGHT**
**ISBN 0 - 908412 - 78 - 9**

Copyright ANGP

**E-MAIL: info@angp.co.za**
**ALL NATIONS GOSPEL PUBLISHERS**
**Posbus 2191, PRETORIA, 0001, R.S.A.**

**(Une Mission de Littérature évangélique financée de dons)**
**(Reg. No. 1961/001798/08)**

## MOYO WA MUTU

Kitabu hiki si kitabu kipya. Kilipigwa kwanza katika inchi ya la France miaka 200 mbele. Kinakwisha kuleta nuru na baraka kubwa kwa elfu za watu. Ni kioo ya roho ndani yake wanaume na wanawake wanaweza kuona hali ya roho zao kama Mungu anavyoiona. Wingi wanakwisha kuona mioyo yao ya zambi, kisha walitubu na kupokea mioyo mipya na roho mpya ndani yao.

Wakati unaposoma kitabu hiki, kumbuka ya kama ni kioo ya moyo wako ndani yake unaweza kusoma na kuyiona mwenyewe. Kama wewe ni mupagano, MuKristiano ao MuKristiano aliyerudi nyuma na kuacha njia ya Bwana, utakuta picha lako kama Mungu anavyoliona. Mungu hana upendeleo na mutu. Anatazama moyo wa muti, si uso wake ao rangi ya ngozi yake.

Satani ni baba ya wawongo wote, mukubwa wa giza na mungu wa dunia hii. Anayigeuza kuwa kama malaika ya nuru, lckini yeye si tena malaika ya nuru kama watu wingi wanavyopenda kumwonesha wanaokasirika wakati Satani anapofunuliwa kwa hali yake ya kweli. Kama zamani, leo vilevile kuna mitume wingi ya uwongo, wenye kutenda kazi kwa hila, wanaoyigeuza kuonekana kama mitume ya Kristo. Wala hatuhitaji kushangala, kwani Satani yeye mwenyewe anayigeuza awe malaika ya nuru. 2 WaKorinto 11:13,14. Satani anapofusha macho na nia za watu hata hawawezi kuona mapendo ya Mungu, utukufu na ukubwa Wake, wala hawawezi kuona Mwokozi wao, Yesu Kristo. 2 WaKorinto 4:4. Macho yao yanapofushwa na mungu wa dunia hii wala hawawezi kuona ya kama wanakimbia kuingia uharibifu wa milele, Hadeze ya milele inayowaka kwa kiberiti. Wao ni wafu mbele ya Mungu na wanatawaliwa na roho ya mungu wa dunia hii. WaEfeso 2:2.

Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alionekana, ili avunje kazi za Satani. 1 Yoane 3:8. Muyinyenyekeze basi mbele ya Mungu, mushindane na Satani, naye atawakimbia ninyi. Karibieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. Yakobo 4:7,8.

Wakati unaposoma kitabu hiki na kuona mapicha ndani yake, unaweza kutazama moyo wako. Tafuta moyo wako na ona hali yake. Kama ukiona moyo wako ni mubaya na mwenye zambi, usikane neno hili wala kulificha, lakini kubali na kiri zambi zako. Kama tukisema kwamba hatuna zambi, tunayidanganya wenyewe, wala kweli si ndani yetu. Tukikiri zambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote. Kama tukisema kwamba hatukutenda zambi, tunamufanya Yeye kuwa muwongo, wala neno lake si ndani yetu. 1 Yoane 1:8-10. Muyinyenyekeze basi chini ya mukono wa uwezo wa Mungu opate kusamehe zambi zenu na kuwasafisha ninyi na damu ya damani ya Yesu Kristo.

Ao unatawaliwa na Mungu ao na Satani. Wewe ni mutumwa wa zambi ao mutumishi wa Mungu. Kama zambi ikitawala maisha yako, usikane ya kama ni hivi. Zaidi lia ku Mungu atakayekufungula kwa njia ya Yesu Kristo aliyekuya katika dunia hii kwa kuokola wenye zambi, kwa kufungula macho ya vipofu, kutuondola katika giza na kuondola giza ndani yetu. Alikuya kutuletea nuru Yake ya mushangalo. Yesu alikuya kutuweka huru toka uwezo wa zambi na wa Satani. Kwa njia Yake tunapata wokovu kutoka ku zambi zetu. Unasimama mbele ya Mungu mutakatifu anayeona na anayeyua siri zako zote na matendo yako yote ya maficho na mafikili yako yote. Huwezi kuyificha wala matendo yako mbele ya Mungu. Mwenye kuweka sikio, hatasikia? Mwenye kufanya jicho, hataona? Zaburi 94:9. Kwani macho Yake ni yulu ya njia za watu, naye anaona mienendo yake yote. Hakuna giza wala kuvuli cha mauti pahali watenda uovu wanapoweza kuyificha. Yobu 34:21,22. Kwani macho ya Bwana yanakimbia huko na huko katika dunia nzima, kwa kuyionesha mwenye nguvu kwa ajili yao walio na moyo mukamifilu mbele Yake.
2 Mambo 16:9; Yoane 2:24.

Funikwa. Heri mutu Bwana asiyemuhesabia uovu, na ndani ya roho yake hila haiko. Zaburi 32:1-5. (Soma vilevile Zabur 51). Yesu anaita hata leo; Kuyeni kwangu, ninyi wote munaosumbuka na wenye muzigo muzito, nami nitawapumzisha ninyi. Matayo 11:28-30.

Heri yeye aliyesamehewa makosa yake, na zambi yake ime.

Copyright ANGP

## 1. PICHA LA KWANZA




Picha hili linaonesha moyo wa mupagano na mwenye zambi, wa mutu wa dunia asiyezaliwa tena anayetawaliwa na roho ya dunia hii na tamaa na aibu ya mwili. Hili ni picha la kweli la moyo wake kama Mungu anavyouona. Macho yake mekundu ni mufano wa ulevi. Soma Mezali 23:29-32. Nani ana huzuni? Nani ana macho mekundu? Wao wanaokawa wakati murefu kwa mvinyo, wao wanaokwenda kutafuta mvinyo iliyochanganywa. Usitazame mvinyo wakati ni nyekundu, wakati inapotia bilauri rangi yake, wakati inaposhuka taratibu. Mwisho wake ni kuluma kama nyoka, kuchoma kama fira. Macho yako yanaona wanawake wageni, na moyo wako utasema maneno yasiyofaya.

Copyright ANGP

Chini ya kichwa unaweza kuona moyo wa mutu na nyama namuna namuna ndani yake waliom ifano ya zambi nyingi na namuna namuna katika moyo wa mutu. Mioyo yetu ni nyumba pahali zambi zetu zinapoikala. Mungu anasema: Moyo wa mutu ni mudanganyifu kuliko vitu vyote, ni mwovu sana, nani anayeweza kuuyua? Yeremia 17:9. Yesu Yeye mwenyewe alisema: Kwa maana ndani ya mioyo ya watu yanatoka mawazo mabaya, matukano, kiburi, upumbafu. Haya yote yaliyo maovu yanatoka ndani, yanafanyiza mutu muchafu.
Marako 7:21-23.

TAUSI:

Nyama ya kwanza ni Tausi. Ni ndege muzuri sana kwa kuonekana na nyoya zake za rangi mbalimbali. Ni mufano hapa wa zambi ya majivuno. Lusiferi, Kerubi aliyepakaliwa (malaika) aliyekuwa zamani mwenye kubeba nuru ya Mungu, malaika ya Mungu, alianguka kwa sababu ya majivuno, aligeuka kuwa adui ya Mungu, Satani. Isaya 14:9-17. Satani si malaika ya giza.

Majivuno yanayionesha kwa njia mbalimbali. Wangine wanayivuna yulu ya mali zao, yulu ya makundi yao ya ngombe, kondolo, nyumba na inchi, yulu ya mavazi mazuri, uso muzuri, na mwili wanaouonesha wazi pasipo haya. Wangine wananuka na majivuno ya kabila, ya mafundisho mingi, ya nguvu ya mwili, na kuendelea katika maneno ya dunia, rangi ya ngozi yao na maneno bulebule mangine mingi. Wangine wanapima kuongeza uzuri wa miili yao kwa njia ya kuvala vikuku na pete za masikio, kwa njia ya kuchanja miili yao na kuikatakata wakati Mungu anapokwisha kuumba mukamilifu. Mungu anashindana na wenye kiburi, lakini anawapa wanyenyekevu neema. 1 Petero 5:5. Mungu anachukia majivuno na kuburi. Mezali 8:13. Kiburi kinatangulia kuangamizwa, na roho yenye kuyivuna inatangulia maanguko. Mezali 16:18.

IMBWA:
Imbwa ni mufano wa tamaa ya mwili, ya uasherati na uzini. Pahali po pote imbwa anapokwenda, anayichafua. Watu wingi wanafanya vivyo. Pahali po pote wanapokwenda wanaanza kucheza na kupendana na wanawake, ao wanawake na wanaume. Uzini na uasherati zinakwisha kuongezeka sana sana kwa siku hizi mbovu za mwisho. Viyana hawayui kuyitawala wenyewe, na hata wanaume na wanawake wanaokwisha kuoana, pamoya na wajane wingi, wanaishi katika uasherati. Zambi ya Sodomo inakwisha kushika maisha za elfu za watu na kutimiza maneno ya Yesu wakati alipotabiri ya kama siku za mwisho zitafanana na siku za Sodomo na Gomora. Watu wa makabila mingi wanaita mutu anayetembela katika uzini na uasherati “IMBWA.” Watu namuna hii hawatariti ufalme wa Mungu, kwani inje ni imbwa, na wachawi, na wazini, na wauaji, na wanaoabudu sanamu, na kila mutu anayependa uwongo na kuufanya. Ufunulo 22:15. Kwa hivi KIMBIA uzini. Kila zambi mutu anayofanya ni inje ya mwili, lakini yeye anayefanya uzini anafanya zambi yulu ya mwili wake mwenyewe. Nini? Hamuyui ya kwamba ninyi ni hekalu la Mungu na Roho ya Mungu anaikala ndani yenu? Kama mutu akiharibu hekalu la Mungu, Mungu atamuharibu yeye, kwa sababu hekalu la Mungu ni takatifu, ninyi ni hekalu lile. 1 WaKorinto 3:16-18).

Copyright ANGP

NGURUWE:
Nguruwe ni mufano wa zambi ya ulevi na ulafi. Nguruwe anakula kila kitu anachokuta njiani. Hachagui kitu kizuri, kama vile watu wingi wanavyokula nyama waliokufa pasipo kuuawa, waliokufa kwa ugonjwa ao waliosongwa kwa kamba. Wanakula damu, panya na nyama wangine Mungu aliotukataza kula. Matendo 15:20; Isaya 66:3-7. Tena wanachafua miili yao, hekalu la Mungu kwa njia ya kuvuta tumbako chafu ao bangi inayochafua na kutia sumu ndani ya damu yao na kuwaongoza kupata desturi za zambi. Satani anawafunga kwa njia ya kuwapa kutaka kukubwa kwa kuvuta, na ni kwa uwezo wa Mungu tu mwanamume ao mwanamuke anaweza kufunguliwa toka desturi hii chafu. Watu, viyana na wazee wanaona ni kitu bule kulewa na malofu ao na malofu ya moto. Lakini hakuna mulevi atakayeriti Ufalme wa Mungu. Malofu si chakula, ni kileo cha sumu kinachoharibu nia ya mutu hata wale wanayoakunywa wanatenda kwa upumbafu, wanafanya zambi katika mwili na wanaweza hata kuua wenzao, kitu wasichoweza kufanya isipokuwa wamekwisha kulewa. Kwani mvinyo ni mwenye kuzihaki, na kileo cha nguvu kinaleta ugomvu; mutu ye yote anayedanganywa nayo hana hekima. Mezali 21:1. Kwa Sheria ya Mose, kama mutu ye yote akikuwa na mwana asiyetii, aliye mulevi, ilimupasa kumwua kwa kumutupia mawe. 2 Torati 21:19-21. Wale wanaopiga malofu na vileo vingine vya nguvu, wana zambi vilevile kama wale wanaoviuza na kivikunywa, kwani Neno la Mungu linesema, Ole kwao wanaochanganya vileo. Isaya 5:22. Ole kwake yeye anayemupa jirani yake kileo, anayemupa chupa, na kumufanyiza kulewa. Habakuki 2:15. Hamuyui ya kama wazalimu hawatariti ufalme wa Mungu? Musidanganywe: waasherati, wala wenye kuabudu sanamu, wala wazini, wala wakike, wala wafirayi, wala wizi, wala

wenye tamaa, wala WALEVI, wala watukanayi wala wanyanganyi hawatariti ufalme wa Mungu. 1 WaKorinto 6:9,10.

Basi matendo ya mwili yanaonekan, ndiyo: uasherati, uchafu, uzini, kuabudu sanamu, ulozi, uadui, ugomvi, uwivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, uuaji wa mutu, ulevi, ulafi, na yanayofanana na maneno haya: yulu ya maneno haya ninawaambia ninyi mbele kama nilivyowaambia ninyi zamani; watu wale wanaotenda maneno ya namuna hii, hawatariti ufalme wa Mungu. WaGalatia 5:19-21. Wala musilewe kwa mvinyo, ndani yake ni makelele, lakini muyalishwe Roho. WaEefeso 5:18. Yesu, kisima cha mayi, ya uzima anaita wenye kiu: Mutu akiona kiu aye kwangu, anywe. Yoane 7:37,38. Haya, kila mutu anayeona kiu, muye kwa mayi, naye asiye na feza, kuyeni, mununue, na kula: ndiyo muye, mununue mvinyo na maziwa pasipo feza na pasipo bei. Kwa nini munatoa feza yenu kwa ajili ya kitu kisicho chakula na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha? Isaya 55:1,2.

KULU:

Nyama huyu anayetembela polepole sana ni mufano wa zambi ya uvivu, kukawia, na uchawi. Kutokuamini ni zambi ya uchawi vilevile. Yeye aliye muvivu anaanguka katika majaribu mingi. Atapenda kuiba zaidi ya kutumika na tena mara nyingi katika kuiba kwake inamupasa kuua mutu. Uvivu katika roho unatuzuiza tusilombe, wala kusoma Kitabu cha Mungu wala kwenda kwa nyumba ya Mungu. Unatuzuiza tusitafute Kitabu cha Mungu ndani yake tuna uzima wa milele. Kukawia ni kama mwizi anayeiba wakati muzuri na kunafikisha mwenye kukawa kwa uharibifu. Wakati Mungu ana anapokwisha kusema nawe kumupa moyo wako leo, Satani anafika mbio na kukuambia kungoya kwanza na kufanya hivi kesho ao siku nyingine, lakini hakose siku ile nyingine haitakukuta ku dunia. Unakawa siku moya, siku nyingine, mwaka mumoya, mwaka mungine hata wakati mauti inapokufikia wakati usipofikili na unakufa pasipo Mungu, pasipo wokuvu, na pasipo Kristo. Kwa hivi Mungu anasema: Leo kama mutasikia sauti yake, musifanye migumu mioyo yenu. WaEbrania 3:7,8.

Ngamba ya kulu inatumiwa mara nyingi na wafumu, na hivi ni mufano wa zambi ya kutegemea na kutenda ufumu na uchawi wakati inapotupasa kutegemea Mungu aliye hai. Ku pahali pakuitia Mungu aliye hai kwa wakati wa ugonjwa na taabu, watu wanatumainia sanamu, mashina ya mapando, mawe, pembe za nyama na vitu vingine visivyo na uzima mufumu anavyowaambia yulu yao, wakati inapowapasa kuamini Mwumba na Mukombozi wao. Mungu aliagiza wana wa Israeli akisema, "Hutaacha mwanamuke muchawi kuishi. Kutoka 22:18. Asionekane katikati yako … anayetumia maaguzi, anayetenda ubashiri, wala muganga wala muchawi wala mupendezi, wala mutu anayepandisha pepo, wala muchawi, wala mutu anayesema na wafu. Kwa maama mutu ye yote anayefanya maneno haya ni chukizo kwa Bwana. Musiendee wenye pepo wala wachawi; musiwatafute ili muchafuwe nao; mimi ni Bwana Mungu wenu. WaLawi 19:31. Na mutu yule atakayekwendea wenye pepo na wachawi, ili kuzini pamoya nao, nitakazia mutu yule uso wangu na kumukatilia mbali na watu wake. Muyitakase basi muwe watakatifu; kwa kuwa mimi ni Bwana Mungu wenu: WaLawi 20:6,7. Yesu Kristo peke Yake ni Mwokozi wa roho, naisi na mwili, anayesamehe makosa yetu yote na anayeponesha gonjwa zetu zote. Zaburi 103:1-3. Mutu wa kwenu amekuwa na ugonjwa? aite wazee wa kanisa; nao walombe yulu yake, na kumupakala mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kulomba kwa imani kutaokola mugonjwa yule, na Bwana atomusimamisha; na kama amefanya zambi, atasamehewa. Kirini zambi ninyi kwa ninyi, na kulombeana, mupate kuponeshwa. Kulomba kwake mwenye haki kuna faida sana, kama akilomba kwa bidii. Yakobo 5:14-16.

Wakati unaposoma kitabu hiki kidogo, Mungu anasemezana nawe akikuagiza kutubu zambi zako na kutoa maisha yako kwa Mungu, lakini roho ya kulu iliyo ndani ya moyo wako inasema nawana sauti polepole: Usifanye kwa haraka, usiyitoe leo, utaweza kufanya hivi kesho, juma la nyuma ao hata mwaka wa nyuma; ulizana kwanza na bwana yako, ulizana kwanza na muke wako ao baba yako kama watasema nini; oa kwanza na kutahiri watoto wako. Ku pahali pa kutii sauti ya Mungu unaweka masikio yako kusikiliza sauti ya hila ya Satani. Kwa njia ya kufanya hivi, unafanyiza moyo wako kuwa mugumu hata utakuwa mugumu sawasawa na ngamba ya kulu.

Copyright ANGP

CHUI:
Huyu ni nyama mukali sana anayependa sana kuua nyama wangine. Ni mufano wa kasirani, gazabu, na hasira, zilizo ndani ya moyo wa mutu. Kila mutu anayetawaliwa na kasirani ni mbio kutenda maneno mabaya, kutukana na hata kuua mutu mungine. Ni kama mara nyingi mutu anaingiza roho ile ya Satani ndani yake wakati anapokunywa malofu hata hawezi kuyitawala mwenyewe tena. Watu wa woga wingi wanakunywa malofu mingi kwa kupata ukaramisu kutenda mambo mabaya kwa kuyilipia kisasi. Mvinyo yao ni sumu ya majoka. 2 Torati 32:33. Kisasi ni katamu kwa moyo mwenye zambi, lakini Mungu ni mwenye kulipiza kisasi kwa ajili yetu. Yesu alisema: Pendeni adui zenu. Mungu ameahidi kusamehe zambi zetu kama tukisamehe watu zambi zao wanazotutendea sisi.

NYOKA:
Nyama huyu aliyekuwa muzuri sana kwa kuonekana kwake zamani alidanganya Adamu na Hawa katika shamba la Edeni, akaharibu upatano wao mutamu pamoya na Mungu. Satani alikuwa na hasidi wakati alipoona namuna gani Mungu alipenda mwanamume wa kwanza na mwanamuke wa kwanza na namuna gani aliwaweka watawala yulu ya dunia nzima ku pahali pa Lusiferi, Satani. Kwa sababu ya hasidi Satani alifanya shauri, akaweza kuharibu upatano muzuri sana wa mutu pamoya na Mungu. Ile hasidi kali, hasidi inayoweza kukufikisha hata kwa uuaji, ni ndani ya moyo wako vilevile na inakuzuiza kufurahi wakati watu wangine wanapofurahi na wanaikala na salama. Inapasa hata watumishi wa Mungu kufanya ange roho hii ya hasidi, roho ya Satani, isiingie ndani ya mioyo yao, wakati Mungu anapotumika na kubariki mutumishi Wake mungine kuliko wao wenyewe. Hasidi inaweka mafikili mabaya mingi ndani ya moyo wako kwa kuloga watu wangine na kuharibu furaha yao na kuua wale unaowahasidia. Hasidi katikati ya mume na muke inaweza kuharibu nyumba yao na maisha yao. Hasidi ni kali kama kaburi. Wimbo wa Solomono 8:6.

Copyright ANGP

CHULA:
Chula anayikulisha na udongo na ni mufano hapa wa zambi ya choyo, na mapendo ya feza na mali yaliyo shina la ubaya wote. 1 Timoteo 6:10. Kuna vyula wangine katika Congo wanaokula siafu hata kufika saa tumbo lao linapopasuka na wanakufa. Mwenye choyo hayuko tayari kushiriki vitu vyake na wangine na kusaidia masikini na wenye hitaji. Anapima kwa njia yo yote, njia zilizo haki na njia zisizo haki kukusanya na kuyipatia mali za dunia zitakazoharibiwa na kutu na nondo, no kuibwa na wizi. Kwa hivi Yesu alituagiza kuyiwekea hazina mbinguni pahali nondo wala kutu haviharibu, wala wizi hawavunji na kuiba, kwa maana pahali hazina yako iko, pahali moyo wako utakapokuwa vilevile. Matayo 6:19-21. Akana na nyumba yake waliharibiwa kwa sababu alipenda zahabu na feza na mavazi ya bei gali na alikamata vitu vilivyolaaniwa. Yosua 7. Yuda Iskariota, mwanafunzi wa Yesu, aliharibiwa kwa sababu alipenda feza kuliko Yesu. Matayo 25:3-5.

SATANI:
Huyu ni baba ya wawongo wote na wa wote wanaofanya uwongo. Yeye ni muchungayi wa nyama wale wote na mutawala wa moyo wako. Ninyi wa baba yenu Satani, na tamaa za baba yenu munataka kuzifanya. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, na hakuikala katika kweli; kwa sababu hakuna kweli ndani yake. Wakati anaposema uwongo, anasema yaliyo yake mwenyewe, kwa sababu yeye ni muwongo na baba ya wongo. Yoane 8:44.

NYOTA:

Nyota ni mufano wa damiri ndani ya moyo wa kila mutu. Uione hapa, nyeusi, ikikuwa imechafuwa na zambi, desturi mbaya hata haiwezi kufanya kazi yake vizuri. WaEbrania 10:22.

JICHO:

Jicho la Mungu ni pahali po pote naye anaona maneno yote ndani ya moyo. Haiwezekani kuficha kitu mbele ya macho makali ya Mungu. Kwa hivi anayua na anaona mafikili yote ya siri na makusudi yote ya moyo. Hata ukitenda zambi zako katika giza jeusi sana, ao katika mwitu wa kufungana kabisa, ao pahali gani, Mungu anakuona.

MALAIKA:

Malaika ni mufano wa Neno la Mungu. Mungu anasemezana na mwenye zambi anayedanganywa na Satani, anamwambia kutubu na kurushusu nuru ya Mungu kuingia ndani ya moyo wake wa giza. Mungu anasemezana na wewe, musomayi, kwa njia ya kitabu hiki.

HUA:

Ndege huyu safi na mupole ni mufano wa Roho Mutakatifu, roho ya kweli anayeonesha mutu zambi zake na haki ya Mungu na hukumu. Roho Mutakatifu katika picha hili ni inje ya moyo. Hawezi kuikala pahali zambi inapotawala.


NDIMI NDOGO ZA MOTO:

Ndimi ndogo za moto zinazozunguka moyo wa mwenye zambi zinapasha yulu ya mapendo ya Mungu yanayozunguka moyo wa zambi, kwani Mungu hataki mauti ya mwenye zambi, lakini atubu na kuishi. Yesu alikuya kuokola wenye zambi. Furaha ni kubwa sana mbinguni yulu ya mwenye zambi mumoya anayetubu. Mungu anataka kusafisha moyo na damu ya Mwana Wake Muzaliwa pekee, Yesu Kristo. Ndimi ndogo za moto ni mufano wake vilevile. Mapendo ya Mungu yanataka kuingia ndani ya moyo baridi uliokufa kwa sababu ya zambi.

Yesu anasimama kwa mulango wa moyo na anapiga hodi. Kama ukimufungulia mulango, Yeye ataingia, atasafisha moyo wako na kukuweka huru.

Copyright ANGP

## 2. PICHA LA PILI




Picha hili linaonesha mutu anayeanza kutubu na kutafuta Mungu. Malaika anashika upanga, Neno la Mungu, lililo hai, lenye nguvu, na ukali kupita ukali wa upanga unaokata ngambo mbili, lititobola hata kutenga nafsi na roho, na viungu na mafuta ndani ya mifupa; nalo ni yepesi kufahamu mawazo na makusudi ya moyo. WaEbrania 4:12. Neno la Mungu linamukumbusha ya kama mishahara ya zambi ni mauti, na ya kama watu wanawekwa kufa mara moya, na nyuma ya kufa hukumu. WaEbrania 9:27. Sehemu ya mwenye zambi na musiyeamini itakuwa katika tanganyika ya moto inayowaka na kiberiti.

Copyright ANGP

Ndani ya mukono wake mungine malaika anashika mifupa ya kichwa. Neno hili ni kukumbusha mwenye zambi ya kama inatupasa sisi sote kufa. Mwili wetu tunaoupenda sana na kuweka saa nyingi yulu yake kwa kuuchunga na kuulisha na kuuvalisha, utakufa na utaharibika. Vidudu wataukula, na nafsi zetu na roho zetu zitatokea mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Mwenye zambi anaanza kusikiliza maonyo ya Mungu na anafungula moyo wake kupokea mapendo ya Mungu. Roho Mutakatifu anaanza kungala ndani ya moyo wake wa giza. Nuru ya Mungu inaingia, inaanza kufukuza giza lote. Pahali nuru inapoonekana, inapasa giza kukimbia. Moto wa mapendo ya Mungu unaanza kuyeyusha moyo baridi. Zambi tulizozionesha kwa njia ya nyama mbalimbali zinapaswa kukimbia.

Mwenye zambi, ruhusu Yesu, nuru ya ulimwengu, kuingia ndani ya moyo wako, halufu giza na matendo ya giza yatapaswa kuondoka katika moyo wako kama unavyoona katika picha. Yesu alisema, Mimi ni nuru ya dunia; yeye anayenifuata hatakwenda kwa giza kabisa, lakini atakuwa na nuru ya uzima. Yoane 8:12. Ole kwao wanaopenda giza kuliko nuru. Wakati Yesu alipoingia hekalu ku Yerusalema, alifukuza wote waliokuwa wakiuza ngombe, kondolo na hua, na alimwanga mali ya wenye kubadilisha faranka, akasema: Nyumba yangu ni nyumba ya malombi, lakini ninyi muliifanyiza kuwa pango

la wizi. Yoane 2:13-17. Nyumba hii ni moyo wako. Yesu hakuya tu kwa kusamehe zambi zetu, akini alikuya vilevile kutuokola na kutufungula toka uwezo na utawala wa zambi. Kama Mwana basi anawaweka ninyi huru, mutakuwa huru kweli. Yoane 8:36.

## 3. PICHA LA TATU




Hapa tunaona moyo wa mwenye zambi mumoya anayetubu kweli kweli. Anaona na anafahamu ukubwa na ubaya wa zambi zake nyingi kwa ajili yao Yesu alisulibishwa yulu ya musalaba. Wakati anapotazoma musalaba, malaika, Neno la Mungu anaomufunulia, moyo wake unavunjika. Mapendo ya Mungu yanayoonekana ndani ya Kristo Yesu yanayeyusha moyo wake, zaidi wakati anapokumbuka ya kama Yesu Kristo. Mwanakondolo ya Mungu alikuya kuondola zambi zake nyingi na alikuwa tayari kufa kwa pahali pake yulu ya musalaba. Neno hili ya kama Yesu alipigwa, na alitiwa taji ya miiba, na ya kama waliingiza misumari ndani ya mikono na migulu Yake na alitundikwa yulu ya musalaba kwa sababu ya zambi zetu, linavunja moyo wa mwenye zambi anayetubu. Wakati anaposoma na kusikia Neno la Mungu, anayiona mwenyewe ndani ya kioo ya Mungu na anafahamu weusi na ubaya mukubwa wa moyo wake unaoyala na zambi. Neno hili linatobola moyo wake, na roho ya huzuni na mashitiko yulu ya zambi zake inamuliisha kwa sababu ya zambi zake, na Mungu anamukaribia. Mapendo na salama ya Mungu zinaingia ndani ya moyo wake uliosafishwa na damu ya Yesu Kristo na zambi zote. Anaanza kufahamu ya kama Bwana ni karibu nao wote wenye moyo wa kuvunjika na anaokola wale wenye roho ya mashitiko kwa sababu ya zambi. Zaburi 34:18. Anaponesha wenye moyo wa kuvunjika, na anafunga vilonda vyao. Zaburi 147:3. Tena Neno la Mungu linasema, Mutu huyu ndiye nitakayemwangalia, mutu aliye munyonge … anayetetemeka wakati anaposikia neno langu. Isaya 66:2.

Roho Mutakatifu na mapendo ya Mungu yanaingia ndani ya moyo ule unaokwisha kusafishwa. Wakati anapoangalia na imani musalaba na damu ya Yesu iliyomwangika kwa usamehe wa zambi zetu,

Copyright ANGP

anaanza kufahamu ya kama zambi zake zimesamehewa, na anayua kabisa ndani ya moyo wake ya kama damu ya Yesu Mwana wa Mungu inatusafisha na zambi zote. 1 Yoane 1:7. Yeye anayeamini Yesu hatakufa, lakini atakuwa na uzima wa milele. (Some 1 WaKorinto 6:10,11). Ndani ya Yesu tuna ukombozi wetu kwa njia ya damu yake, usamehe wa zambi zetu, sawasawa na wingi wa neema yake. WaEfeso 1:7. Kuna roho mpya sasa ndani ya moyo wake na tangu sasa hapendi tena ulimwengu wala vitu na maneno ya dunia, lakini anataka maneno ya Mungu aliyeyalisha moyo wake na mapendo Yake. Wale nyama, maana zambi zake, ni inje ya moyo wake, hata kama Satani hataki kuondoka na anaikala kuangalia nyuma akitoraji kupata njia kuingia tena. Kwa hivi tunaagizwa kuangalia na kulomba, na kushindana na Satani hata atukimbie.

## 4. PICHA LA INE

Picha hili linaonesha moyo wa MuKristiano anayekwisha kupata salama na ukombozi kwa nija ya sadaka ya Bwana yetu na Mwokozi Yesu Kristo. Hayisifu yulu ya kitu ila musalaba wa Bwana yetu Yesu Kristo, kwa yeye dunia hii imsulibiwa kwake, na yeye kwa dunia. Wa Galatia 6:14. Anafahamu kabisa ya kama Yesu alikufa yulu ya musalaba hata sisi vile tuwe wafu kwa zambi na tuishi kwa haki. 1 Petero 2:24. MuKristiano amesulibiwa kwa dunia. Tunaagizwa kutembela ku roho pasipo kutimiza tamaa za mwili. WaGalatia 5:12-25. Tena tunaagizwa kufuata utakaso, pasipo huu, hapana mutu atakayeona Mungu. WaEbrania 12:14.

Ndani ya moyo wa picha hili unaweza kuona muti yulu yake walifunga Yesu na kamba nyuma ya kumwondolea mavazi Yake. Unaweza kuona vilevile fimbo walizomupiga nazo pasipo huruma, kwa sababu azabu iliyotupasa sisi kupata ilimwangukia Yeye. Isaya 53:11-12. Alipigwa kwa sababu ya zambi zetu. Mufalme Herode na watu wake walimuzihaki, na nyuma ya kumupiga fimbo walimuvalisha vazi jekundu. Wakati waliposokota taji ya miiba, waliiweka yulu ya kichwa Chake ku pahali pa taji ya zahabu. Waliweka matete ndani ya mukono Wake wa kuume ku pahali pa fimbo ya mufalme. Walipiga magoti yao mbele Yake, wakamuzihaki na kusema, Salamu, mufalme wa WaYuda. Walimutemea mate, waliondosha matete mukononi Mwake, wakapiga kichwa Chake nayo. Nyuma ya kumaliza kumuzihaki walimupeleka kwa kusulibiwa. Kuna watu wingi wakati wa sasa wanaoyiita WaKristiano, wanaolomba ndani ya nyumba za Mungu, wanaovunja Mukate, na kuimba nyimbo za Mungu, lakini kwa matendo yao mabaya wanasulibisha Mwokozi wao tena. Si kila mutu anayeniambia: Bwana, Bwana, atakayeingia ufalme wa mbinguni, lakini yeye anayefanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Matayo 7:21-27. Unaweza kuona mufuko wa faranka wa Yuda ndani ya picha hili. Yuda alitoa Yesu ku mikono ya adui Zake, akamwuza kwa vipande 30 vya feza kwa sababu mapendo ya mali yalipofusha macho yake, na kutawala moyo wake mwovu. Tala, minyororo na vitu vingine vilitumiwa na askari waliokamata Yesu usiku. Mawe ya kupiga kura zilitumiwa na askari vilevile wakati walipopiga kura yulu ya mavazi Yake, wakitimiza unabii wa Mungu: Wanagawa nguo zangu katikati yao, na vazi langu wanalipigia kura. Zaburi 22:18.

Copyright ANGP




Na mukuki askari mumoya alitobola mbavu Zake na moyo Wake na damu na mayi yalitoka. Yoane 19:33-37. Mbele ya kuwika kwa yogolo Petero alikana Yesu mbele ya kijakazi, lakini nyuma alitubu na machozi machungu. Wewe unakiri Yesu kwa njia ya masemo na matendo yako? Ao unaogopa kufnaya hivi? Yesu alisema: Kila mutu anayenikana mbele ya watu, nitamukana vilevile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. Matayo 10:32-33. Yesu alisema tena: Mutu akitaka kunifuata, ayikatale mwenyewe, achukue musalaba wake na kunifuata. Matayo 16:24. Naye asiyechukua musalaba wake na kunifuata hanistahili. Matayo 10:38.

Copyright ANGP

Milele Wewe, Yesu, yuko jiwe la nguvu,
Ulishinda Satani, vile kufa na zambi;
Sasa unisafishe, haki Yako unipe.

## 5. PICHA LA TANO




Hapa tunaona maisha ya mwenye zambi anayekwisha kusafishwa na kutakazwa kwa nijia ya neema kubwa na rehema ya Mungu. Ni sasa hekalu la kweli la Mungu, ikalo la Mungu Baba, Mwana na Roho Mutakatifu, sawasawa na picha la Yesu Kristo: Kama mutu akinipenda atatii neno langu, na Baba yangu atamupenda, nasi tutakuya kwake na tutafanya maikalo yetu kwake. Yoane 14:23. Mungu anaheshimu na kubariki na kutukuza watu kwa njia ya Yesu Kirsto. Luka 1:52.

Moyo unakwisha kugeuka sasa kuwa hekalu la Mungu aliye hai. Zambi inakwisha kuondolewa, Kwa pahali pa nyama mbali-mbali, wanaotawaliwa na Satani baba ya wongo, tunaona Roho Mutakatifu akiikala moyoni. Kwa pahali pa matendo mabaya ya mwili, moyo unakwisha kugeuka kama shamba la kuzala vizuri sana, kama muti mwenye kuzala matunda mingi, ukizala matunda ya Roho kama mapendo, furaha, salama, uvumilivu, neema, wema, uaminifu, upole, uyizuiza, na matunda mangine yanayopendeza Mungu na watu. Anakwisha kugeuka sasa kuwa tawi la kweli linalozala la Muzabibu wa kweli, Bwana yetu Yesu Kristo.

Copyright ANGP

Siri ya kuzala matunda ni kwa mutu kuikala ndani ya Yesu Kristo na Kristo ndani yake. Yoane 15:1-10. Anachunga Neno Lake moyoni mwake vilevile. Akiyalishwa na kubatizwa katika Roho Mutakatifu ana uwezo kushinda mwili na tamaa zake na kusulibisha mwili na kutaka kwake. Kwa uwezo wa Roho Mutakatifu anaweza kutembela ku Roho. Haishi tena kwa njia ya maneno anayoona na kusikia, lakini anaishi kwa imani; maana imani katika Yesu Kristo ni kushinda kunakoshinda dunia. Anaishi kwa taraja na anapatishwa nguvu kwa njia ya taraja iliyo hai ya kama kurudi kwa Bwana yetu Yesu Kristo ni karibu. Anaishi kwa na katika mapendo ya Mungu yanayoikala milele.

Heri wenye moyo safi: maana wao wataona Mungu. Matayo 5:8. Mufalme Daudi hata akikuwa tajiri sana na mwenye kushinda adui zake, hata kama aliua Goliyata, yule mutu murefu sana na watu wangine vilevile, alifahamu hitaji kubwa la maisha yake kama akitaka kuona Mungu. Alilia kutoka katika moyo wake: Umba moyo safi ndani yangu, Ee Mungu, na fanya upya roho nzuri ndani yangu. Zaburi

51:10. Hakuna mutu anayeweza kusafisha moyo wake yeye mwenyewe ao kuumba na kusafisha moyo wake kwa kupima yeye mwenyewe. Sharti afike karibu na Mungu na toba ya kweli na kukiri na kuacha zambi zake kama Mufalme Daudi alivyofanya na kama vilevile mwana mupotevu alivyoacha nguruwe zake na alirudi kwa baba yake na kusema na roho ya kutubu kweli kweli: Baba, milikosa yulu ya Mungu na yulu yako. Mungu ni tayari kabisa kusaidia kila mwenye zambi anayerudi Kwake na roho ya kweli ya toba kwani ni Mungu aliyeahidi na kusema: Nitawapa ninyi moyo mupya, na nitatia roho mpya ndani yenu, nitaondosha moyo wa jiwe katika mwili wenu, nitaweka roho yangu ndani yenu na kuwafanyiza ninyi kutembela katika amuri zangu. Hili ndilo agano jipya Mungu analokwisha kufanya na kutia muhuri kwa damu ya Mwana Wake Yesu Kristo.

Katika picha hili tunaona malaika akitokea tena vilevile. Malaika wanatumikia wale watakaoriti uzima wa milele na wana zunguka wale wanaoogopa Bwana. Zaburi 34:7; 91:11; Danieli 6:22; Matayo 2:13; 18:10; Matendo 5:19; 12:7-10. Satani vilevile anaonekana katika picha hili akisimama karibu na moyo akitafuta njia kuinga katika ikalo lake la mbele. Hivi tunaagizwa kuangalia na kulomba kwa sababu Satani, adui yetu kama simba ya kunguruma anazungukazunguka akitafuta mutu amumeze. 1 Petero 5:8. Mushindane na Satani, naye atawakimbia ninyi. Yakobo 4:7.

## 6. PICHA LA SITA

Hili ni picha la huzuni linaloonesha MuKristiano anayerudi nyuma. Anaanza kufunga jicho moya, kwa kuonesha ya kama anaanza kupola na kulala katika maisha yake ya MuKristiano. Jicho lake la pili linaangalia pahali po pote pasipo haya likitafuta kufanya urafiki na dunia. Nuru ndani ya moyo wake inapunguka, na alama katika mwili wake zilizoonesha ya kama yeye ni tayari kubeba mateso pamoya na Kristo zinakwisha kupunguka wala hazionekani tena zaidi. Yeye ni katikati ya majaribu yanayomushinda polepole wakati ilipomupasa kushindana na Satani. Anasikiliza sauti ya mujaribu, hapana sauti ya Mungu. Hata kama akifika kwa nyumba ya Mungu na anapima kuficha mapendo yake kwa maneno ya dunia ndani ya moyo wake, anakwenda mbali kupita na Mungu wakati wote na mapendo yake ya kwanza kwa Mungu yanakwisha kupotea. Hafikili tena kuchunga moyo wake, lakini anamupa mujaribu anayeikala karibu nafasi.

Roho ya tausi inaanza kupima kuingia. Anapata majivuno, hakose anayivuma hata kwa sababu yeye ni MuKristiano, na anasahabu ya kama ameokolewa kwa neema tu. Ulevi unapiga hodi kwa mulango wa moyo wake vilevile, unapima kuingia. Hakose mutu mungine anamujaribu kunywa kidogo tu ao anamwambia ya kama malofu yasiyo malofu ya moto si neno. Hafahamu ya kama hata mvinyo kidogo ao malofu kidogo ni kama mutoni unaoongoza mutu kufika kwa muto mukubwa wa ulevi. Ao hakose mwanamuke anafanya malofu kwa mume wake na rafiki zake.

Copyright ANGP



Copyright ANGP

Hata akitoa uzuru kusema yeye mwenyewe hakunywi ya malofu yale, yeye ana kosa vilevile kwani anaongoza wangine kuyakunywa na kudanganywa na roho ya ulevi. Uzini na uasherati zinakuya na kujaribu MuKristiano na mayele yote ya Hadeze. Hakose anaanza kusikiliza na furaha masemo machafu na maovu na anaanza kufurahi kuchanganyana na watu wa zambi na kufika pahali pa michezo mibaya. Hakose wangine wanamwambia ya kama kucheza kwa wanaume na wanawake pamoya si zambi, lakini ya kama kucheza namuna ya washenzi ndiyo zambi. Hafahamu ya kama pahali pote pa michezo ni pahali pa zambi na ya kama michezo ya wazungu ni hata miovu kuliko michezo ya washenzi. Kuvuta tumbako na cigarettes ni kubaya kama vilevile kuvuta namuna watu wa zamani walivyovuta, kwa sababu sasa watu wanavuta hata kuliko, muchana na usiku. Yesu hakuvuta tumbako hata mara moya na haifayi MuKristiano anayefuata Yesu kweli kufanya hivi.

Satani anamwambia ya kama kucheza na zambi si zambi. Kufanya zambi mara moya, kufanya tendo moya la zambi si vibaya, ni neno mujaribu analomwambia, hata daimoni ya uovu inakwisha kupata njia kuingia katika moyo unaokwisha kusafishwa na anaikala pale tena.


Yule mutu katika picha hili anayetobola moyo na mukuki ni mufano wa wenye kuzihaki na kushindana na imani ya WaKristiano na masingizio yao. MuKristiano hawezi kuvumilia kuzihaki na kuzarau kwa watu, zaidi kwa rafiki zake. Maneno yao yanatobola moyo wake na kwa sababu mapendo ya Mungu yamepola anaanza kuogopa watu kuliko Mungu, na kwa sababu anaogopa maneno watu wanayosema na kufikili anageuka mutumwa wa watu na anarudi nyuma katika imani yake.

Hasira na kasirani zinatokea tena kwa wakati wa matata na taabu na zinapima kutawala moyo wake, na matukano yanachafua midomo yake aliyoitumia mbele kusifu Mungu na kulomba Kwake. Kama Satani akipata nafasi kidogo tu, mulango kidogo tu, moshi wa hasidi utaingia na kuongeza ukubwa wa mulango kwa kuyapa makosa mangine njia kuingia vilevile.

Ni nyepesi sana kuacha mapendo ya feza kuingia moyoni vilevile isipokuwa tunatii maonyo ya Bwana Yesu aliyesema, Angalieni na kulomba, musiingie katika majabriu. Matayo 26:41. Basi yeye anayezani

anasimama, aangalie asianguke. 1 WaKorinto 10:12. Inatupasa kuvala silaha nzima ya Mungu, hata tuweze kushindana na Satani. WaEfeso 6:11-18.

## 7. PICHA LA SABA




Picha hili linaonesha hali ya moyo wa mutu anayekwisha kurudi nyuma, aliyetiwa nuru ya Habari Njema na kuonja zawadi ya mbinguni, na aliyefanyizwa mushiriki wa Roho Mutakatifu lakini anakwisha kuanguka. Inaonesha vilevile hali ya mutu asiyetubu hata mara moya, hata kama anakwisha kusikia Haban Njema ikihubiriwa tena na tena, lakini aliyefanyiza moyo wake kuwa mugumu na kuendelea katika zambi.

Copyright ANGP

Yesu Yeye mwenyewe alifundisha yulu ya hali ya mwenye kurudi nyuma wakati aliposema: Wakati pepo muchafu anapotoka mutu, anatembela kati ya pahali pasipo mayi, akitafuta pahali pa kupumzika, asipopata, anasema: Nitarudi katika nyumba yangu nilipotoka. Naye akikuya, anaona imefagiwa, imepambwa. Halafu anakwenda kuchukua pepo saba walio waovu kupita yeye mwenyewe: nao wanaingia kula na kuikala; na hali ya mwisho ya mutu yule ni mbaya kuliko ya kwanza. Luka 11:24-27.

Lakini imetokea yulu yao sawasawa na hadizi ile ya kweli: Imbwa amerudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudia kugaagaa ndani ya matope. 2 Petero 2:22.

Mashairi haya yanaonesha wazi hali ya moyo wa mutu huyu. Zambi na udangayifu wake wote imefika kuikala na kutawala moyoni mwake. Ni kama hata ku uso wake kugeuka kwa hali yake ya roho kunaonekana. Ilipasa Roho Mutakatifu kuondoka moyoni kwani zambi na Roho Mutakatifu hawawezi kuikala pamoya. Nuru na giza hayana ushirika hata kidogo. Moyo hauwezi kuwa hekalu la Mungu na pango la Satani vilevile. Malaika, Neno la Mungu, anapaswa kuondoka na huzuni, akiangalia nyuma yake na taraja ya kama mutu huyu atatubu hata sasa kama mwana mupotevu aliyefahamu upumbafu wake wakati alipoketi katikati ya nguruwe na alitaka kuyalisha tumbo lake na chakula cha nguruwe,

lakini hakuna mutu alioyemupa. Alifahamu hali yake ya kurudi nyuma, ya kupotea, akatubu, akasema: Nitaondoka na kwenda kwa baba yangu na kumwambia: Nimekosa mbele ya Mungu na mbele yako, wala sisitahili kuitwa tena mwana wako. Kwa sababu alitubu kweli kweli na aliona huzuni kweli kwa sababu ya zambi ake, baba yake alimusamehe, akaua ndama ya mafuta mingi, akamupokea tena kama mwana. Lakini hakuna roho ya toba kusaidia mutu huyu kurudi karibu na Mfungu, kuanguka kwa migulu ya Yesu, kutafuta usamehe na kusafishwa. Ni kama damiri yake imechomwa kwa moto na inakwisha kufa. Ana masikio kwa kusikia lakini hawezi kusikia sauti ya kusihi ya Mungu tena. Ana macho kwa kuona lakini hawezi kuona shimo pasipo mwisho ya Hadeze ndani yake ataanguka bado kidogo. Hana haya wala huzuni tena lakini anaendelea katika zambi zake waziwazi. Satani anakwisha kuya kutawala moyoni mwake, na anaikala kama mufalme yulu ya kiti chake cha ufalme. Hakose mutu huyu anayisifu hata sasa yulu ya kuonekana kwake kama kaburi linalopakaliwa na pembe, lakini linaloyala ndani na mifupa ya wafu na uchafu wa zambi. Matayo 23:27. Baba ya wongo anakwisha kukamata pahali pa Roho ya kweli. Kila nyama, kila zambi ana daimoni yake na roho yake muchafu kwa kumusaidia kutawala moyo. Hata akitaka kuyifungula toka mikono ya watesi wale wachafu, hawezi, lakini yeye ni mutumwa tu. Anaona kweli ya maneno Mungu aliyosema kwa njia ya Mutume Petero ya kama yeye aliyezarau sheria ya Mose alikufa, na ya kama inapasa azabu kubwa zaidi kwa mutu yule aliyekanyaga Mwana wa Mungu, na kuhesabu damu ya agano aliyotakaswa nayo kuwa kitu kichafu, na kutukana Roho ya neema. WaEbrania 10:29-31; 2 Petero 2:1-14.

Musomayi, kama hii ni hali ya moyo wako lia mbele ya Mungu toka ndani ya nafsi yako. Yeye anaweza na anataka kukuokola, kukusamehe na kukusafisha na zambi zote kama ukifika na roho ya toba ya kweli. Anaweza kufunga Satani na jeshi lake lote na kumufukuza toka moyo wako kama wewe ni tayari kumuruhusu kufanya hivi. Kuya kama mukoma aliyefika ku Yesu na kulia: Kama ukitaka unaweza kunisafisha; na Yesu alisema: Ninataka, safishwa. Marako 1:40-43. Lakini kama unazidi kufanyiza moyo wako kuwa mugumu na unapenda giza kuliko nuru, hakuna taraja wala kusaidia kwa wewe, kwa sababu unachagua mauti ku pahali pa uzima, giza kwa pahali pa nuru.

Copyright ANGP

## 8. PICHA LA NANE


Hapa tunaona mwenye zambi aliyefanyiza moyo wake kuwa mugumu akikaribia mauti, mwili wake ukiyala na kuluma, na nafsi yake ikiyala na woga kwa sababu ya mauti inayokaribia Mauti (mifupa ya mufu, baba ya mifupa), imefika kwa wakati asipofikili wala asipoitaka, na kumutazama na macho makubwa na ya kuogopesha. Furaha ya zambi imepita; sharti afute sasa mishahara mikubwa na ya kuogopesha ya zambi. Umivu wa Hadeze unashika nafsi yake na roho yake zinazoogopa sana. Hata akitaka kulomba, anaona hawezi kufika karibu, na Mungu hamusikii. Maneno yote ya bule bule ya faraja, ya rafiki zake za dunia hayawezi kumusaidia, na mali zake alizolokota kwa sababu ya mapendo yake kwa feza haziwezi kuokola nafsi yake ao kupunguza kuluma ao kuongeza arefu wa maisha yake. Hata akipima kufikili yulu ya Mungu, Satani hamupi njia. Ni kama kila kitu alichopenda katika dunia hii na kwa sababu yake aliishi, kinamuzihaki, na hata wachungayi wake wa uwongo, wa dunia, hawawezi kumusaidia. Anaanza kufahamu ya kama ni kitu cha kuogopesha kuanguka mikononi mwa Mungu aliye hai. Alitaraji atatengeneza maneno yake na Mungu wakati kufa kwake kutakapokaribia, lakini anaona sasa saa hapana.




Elfu za watu wanakufa kwa gafula pasipo kupata njia kutafuta Mungu mbele ya kufa kwao. Kwa hivi tunaagizwa kutafuta Mungu wakati anapoweza kupatikana. Ku pahali pa kusikia maneno ya faraja, ndiyo maneno ya Mungu wakati wa kufa kwake, mutu huyu aliyekatala neema na mapendo ya Mungu kwa wakati wa maisha yake atasikia sasa sauti ya Mwamuzi wake ikisema, Ondoka kwangu wewe uliyelaaniwa, uende katika moto wa milele uliotengenezwa kwa Satani na malaika zake. Matayo 25:41. Na sawasawa watu wanavyowekwa kufa mara moya, na nyuma ya kufa hukumu. WaEebrania 9:27.

Copyright ANGP

9. PICHA LA TISA




Hapa tunaona picha la MuKristiano wa kweli akivumulia na akishinda mateso makali na majaribu ya mwili na ya Satani. Anajaribiwa pande zote, lakini anavumilia hata mwisho. Yeye ni mushinda na kupita mushinda katika Yesu Kristo. Hakuanza tu katika mashindano ya imani yake, lakini anayamaliza vilevile akitazama Yesu mwenye kuanzisha na mwenye kutimiliza imani yetu, WaEbrania 12:1,2.

Satani na jeshi lake lote wanazunguka moyo wa mutu anayeamini wakipima kupata njia kuingia, lakini hawapati. Majivuno, mapendo ya feza, zambi za mwili zinapiga hodi. Ku pahali pa imbwa na chui tunaona “Mbuzi ndume na punda,” kwani mara nyingi zambi inageuza sura yake ao jina lake. Lakini MuKristiano anayeangalia kabisa anatambula zambi ku kila sura, hata ikibeba jina la dini, ao ikionekana kama malaika ya nuru, kwani Neno la Mungu na Roho ya kweli ndani ya moyo wake wanamwongoza katika kweli yote na kumusaidia kutambula ubaya na uzuri. Pamoya na nyama wale wote na daimoni zao, unaweza kuona mutu mumoya akicheza mbele yake na kopo ya mvinyo ao malofu mukononi mwake na akiita MuKristiano kushiriki ndani ya furaha za dunia hii na ndani ya malofu na michezo. Lakini maneno haya yote ni bule kwa MuKristiano anyekwisha kuyitoa kwa Bwana na anayekwisha kufa kwa maneno ya zambi na kwa dunia. Yanamusukuma karibu kupita na Mungu. Yule mutu mungine anamutobola na mukuki. Masemo mabaya, masingizio, zihaka na maneno ya kuogopesha, zaidi kwa njia ya mwasioamini, lakini mara nyingine kwa njia ya watu wanayoiita WaKristiano yanatobola moyo wake. Lakini anayifariji na maneno ya Yesu aliyesema, Heri ninyi wakati watu wanapowatukana ninyi na kuwatesa ninyi na kuwasemea ninyi kila neno baya kwa uwongo, kwa sababu yangu. Furahini, shangilieni, kwa sababu zawabu yenu ni kubwa mbinguni. Matayo 5:11,12.

Zambi, mwili, ndio umutu ndani yake, na Satani wanapima sana kugawa MuKristiano na mapendo ya Mungu. Lakini na ukaramisu wote anaweza kusema: Ni nani anayetutenga na mapendo ya Kristo? Mateso, ao taabu, aa ufukuzo, ao njala, ao utupu, ao hatari, ao upanga? Lakini katika mambo haya yote tunashinda na zaidi ya kushinda, kwa njia ya mwenye kutupenda. WaRoma 8:35-39. Akikuwa amevala silaha yote ya Mungu anaweza kusimama katika siku mbaya na kwa uwezo wa Roho Mutakatifua anashinda tamaa ya mwili na majaribu yote mangine. Anafahamu ya kama Kristo anayeishi ndani ya moyo wake ana uwezo kuliko Satani na jeshi lake, maana Yeye aliye ndani yetu ana nguvu kuliko yeye aliye katika dunia, ndiye, Satani. Yesu Kristo alishinda Satani, zambi na mauti na kwa njia yake tunageuka wenye kushinda na zaida ya kushinda, na tunaweza kushinda na kupata taji ya utukufu.

Nyota ya damiri yake ni safi na inangala. Moyo wake unayala na imani na Roho Mutakatifu. Malaika ya Mungu yulu yake anamukumbusha ahadi nzuri sana wanazopewa wale wanaoshinda na kuvumilia hata mwisho. Utunulo 2:7,11,17,26; 3:5,13,21.

Mufuko wa feza ulio wazi unaonesha ya kama si moyo wake tu lakini feza yake na vitu vyote alivyo nayo vinatolewa kwa Mungu. Ku pahali pa kupoteza mishahara yake katika furaha za zambi, anasaidia masikini, anatoa sehemu moya ya kumi ya yote anayopata kwa Mungu pamoya na kusaidia pahali po pote anapoweza na sadaka nyingine. Katika kila njia anatumia mali yake kwa utukufu wa Mungu, kama kondolo aliye tayari kutoa manyoya yake. Muzigo wa mukate na samaki unaonesha ya kama anatembela safi, pasipo ulevi na ulafi. Hafanyi malofu wala mvinyo kuwa chakula chake wala havuti tumbako kwani anakumbuka ya kama inamupasa kuchunga mwili wake safi kama hekalu la Mungu. Moyo wake mwenyewe unakwisha kugeuka nyumba ya malombi, lakini anafikaga ku nyumba ya Mungu vilevile kila mara hata wakati yeye mewenyewe anapochoka ao mvula inapoanguka. Anapenda malombi, ao katika nyumba ya Mungu, ao katika chumba chake mwenyewe. Anakutanisha watu wa nyumba yake kila siku kwa malombi kwani anayua MuKristiano hawezi kuishi pasipo malombi, kama vilevile samaki hawezi kuishi pasipo mayi. Kitabu kilicho wazi kinaonesha ya kama Biblia, Neno la Mungu ni Kitabu wazi mbele yake naye anakisoma na kutafuta ndani yake na roho yote. Ni tala kwa migulu yake, ni upangan kwa kushinda nao Satani, ni chakula chake cha kila siku, chakula cha roho kinachomupatisha uzima, ni mayi kumaliza kiu yake. Mara nyingine anaoga kabisa ndani ya Neno la Mungu na analitumia kama kioo kwa kumwonesha hali ya moyo wake.

Copyright ANGP

Anapenda kubeba musalaba, unaomukumbusha ya kama yeye mwenyewe amesulibiwa pamoya na Kristo na amefufuliwa kutembela katika upya wa uzima, na hivi anatafuta maneno yaliyo yulu, maneno yaliyo ya milele, maneno yasiyoonekana kwa macho. Yeye ni tayari kukutana na Mungu na ni kama muti unaopandwa kando ya mayi unaozala matunda yake kwa wakati wake, kama tawi katika ule muzabibu wa kweli akizala matunda. Mapendo ya kutimia ya Mungu yameyalisha moyo wake, na hivi haogopi mauti. Zaburi 1:1-3; Yoane 15:114; 1 Yoane 4:18-21.

## 10. PICHA LA KUMI




Copyright ANGP

Yesu alisema: Mimi ni ufufuko na uzima: yeye anayeniamini hata anapokufa, ataishi: na kila mutu mwenye uzima na kuniamini mimi hatakufa hata milele. Yoane 11:25,26. Yeye anayesikia neno langu na kumwamini yeye aliyenituma ana uzima wa milele; hafiki kwa hukumu, lakini amepita kutoka mauti kuingia uzima. Yoane 5:24. Mauti haiwezi kuogopesha wala kutesa MuKristiano, kwani mauti imemezwa kwa kushinda. Ee mauti, kushinda kwako ni wapi? Ee mauti, uchungu wako ni wapi? Asante kwa Mungu anayetupa sisi kushinda kwa Bwana yetu Yesu Kristo. 1 WaKorinto 15:54-57.

Mutu anayekwisha kuishi kwa Mungu haogopi kufa. Wakati saa ya kuondoka kwake katika dunia inapokwisha kufika anakwenda na furaha kwa ikalo lake la milele. Mutume Paulo alisema: Nikitamani kwenda zangu niikale pamoya na Kristo: maana ni vizuri zaidi sana. WaFilipi 1:23. MuKristiano ana hamu sana kuona uso wa Yesu aliyemukufilia yulu ya musalaba na kumukombola na damu Yake mwenyewe. Roho Mutakatifu anamukumbusha maneno ya Yesu wakati aliposema: Musifazaike mioyoni mwenu: munaamini Mungu, muniaamini mimi vilevile: Katika nyumba ya baba yangu ni maikalo mingi. Nitakuya tena, na nitawakaribisha ninyi kwangu; pahali ninapoikala mimi, mwikale vilevile. Yoane 14:1-4. Jicho halikuona, wala sikio halikusikia, wala hayakuingia katika moyo wa mutu maneno Mungu aliytengenezea wenye kumupenda. 1 WaKorinto 2:9. Hakuna lugha duniani inayofaya kueleza ao kuonesha utukufu wa pahali pa mbingu panapotayarishwa kwa wale wanaoshinda hapa duniani na kuemini Bwana Yesu Kristo.

Katika picha hili la kumi tunakumbushwa yulu ya kwenda kwake mbinguni kwa kila mwamini wa kweli. Ku pahali pa mifupa ya kuogopesha ya mufu, tunaona malaika ya Mungu. Yeye anangoya kupeleka roho inayokwisha kuhesabiwa haki karibu na Mungu. Nafsi na roho zinafunguliwa chini ya muzigo wa

mwili wa kufa na zinafika Kwake aliyemupenda na kwa njia yake aliisha na kufa hapa duniani. Mungu atamukaribisha na furaha sana Kwake, atamwambia: Vema, mutumwa mwema na mwaminifu; ingia katika furaha ya bwana yako. Matayo 25:21. Satani hana uwezo yulu yake tena kwani ni ya damani machoni mwa Bwana mauti ya watakatifu wake. Zaburi 116:15. Nikasikia sauti toka mbiguni ikisema: Andika, Heri wafu wanaokufa katika Bwana tangu sasa. Ndivyo, anasema Roho, wapate kupumzika nyuma ya taabu zao; na matendo yao yanafuatana nao. Ufunulo 14:13.

## LAST ADMONITION

Musomayi mupenzi wa kitabu hiki, Mungu akusaidie kutoa moyo wako kwa Yesu, kwani anasema, Mwana Wangu, binti Yangu, unipe moyo wako. Atakupa moyo safi na kuweka roho nzuri ndani yake. Usiache moyo wako wa udanganyifu kukuongoza kwa njia mbaya, kwa njia ya kufuata tamaa mbaya, kwani yeye anayetegemea moyo wake mwenyewe ni mupumbafu. Mezali 28:26. Lakini yeye anayetembela na akili ataokolewa Acha zambi zako na fungana na haki, kwani mishahara ya zambi ni mauti, lakini zawadi ya Mungu ni uzima wa milele kwa Yesu Kristo.

Na wewe unayekwisha kuweka maisha yako mikononi mwa Mungu, shika nguvu mafundisho mema, katika imani na mapendo yaliyo katika Kristo Yesu, kwani unayua yeye uliyemwamini, na unayua kabisa ya kwamba anaweza kulinda ile uliyoweka kwake hata siku ile. 2 Timoteo 1:12. Uyiyenge katika imani iliyo takatifu zaidi, ukilomba ku Roho Mutakatifu, uyichunge katika mapendo ya Mungu, ukitazamia Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiliza imani yetu, Yeye Mufalma atakayekuya bado kidogo.

Na sasa yeye anyeweza kuwalinda ninyi musiyikwale, na kuwasimamisha ninyi mbele ya utukufu wake pasipo kilema katika furaha kubwa; Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu, kwa Yesu Kristo Bwana yetu; utukufu ni wake, na ukubwa, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele.
Amina. Yuda 24,25.

Copyright ANGP

A SPECIAL WORD FROM ANGP
UN MONDE SPÉCIAL DE L'ANGP
UMA PALAVRA ESPECIAL DA ANGP

This booklet "The Heart of Man" is available in over 538 languages and dialects spoken throughout the world (Africa, Asia, The Far East, South America, Europe, etc.) Our Heart Book is now also available on cell phones, tablets, etc from www.angp-hb.co.za or as an APP "Heart of Man" on Android phones.

Le livre du "Coeur de l'homme" peut etre obtenu en plus de 538 langues et dialectes parles dans le monde entier, a savoir: Afrique, Amerique, Asie, Extreme Orient, Europe. Notre Livre du Coeur est maintenant aussi disponible sur votre Telephone cellular, plaques, etc. de www.angp-hb.co.za ou comme une Application "Heart of Man" sur telephones Android.

Este livro "O Coracao do Homem" e obtfdo em mais de 538 linguas e dialectos falados em todo o mundo, a saber: (Africa, Asia, America do Sul, Extremo Oriente, Europa, etc). O nosso Livro O Coração do Homem tambem esta agora disponivel em telefone celular, tablets, etc. de www.angp-hb.co.za ou como um aplicativo "Heart of Man" nos telephones celulares Android.

Copyright ANGP

The 10 heart pictures contained in this booklet are also available in the form of large coloured picture charts (86 x 61cm) bound together in a set of 10 pictures. These "Heart Charts" can be obtained with European or African features and are particularly suitable to be used in conjunction with the Heart Book for class-teaching, open air evangelization etc. Kindly contact us to ascertain the latest subsidized price of this chart.

Les 10 images du coeur qui figurent dans ce livre peuvent etre obtenues en tableaux de couleur, format 86 x 61 cm, avec des physionomies europeennes ou africaines. Ils peuvent etre utilises en meme temps que le livre du coeur pour des classes bibliques, a l'ecole du dimanche ou lors de reunions de plein air. Soyez aimable de nous contacter pour assurer les derniers prix en cours du tableau.

As 10 imagens do coracao, contidas neste livro podem ser obtidas num conjunto de 10 imagens em colorido no tamanho de (86 x 61 cm). Estes "Cartazes do Coracao podem ser obtfdos com caracterfsticas Europeias e Africanas e podem ser usados em conjuncao com o mesmo livro em classes de ensino biblico, evangelizacao ou ao ar livre. Agradeciamos que nos contacta- se para confirmacao do ultimo preco dos cartazes.



Kindly write to us if you are able to assist us with further translations of our free Gospel literature, informing us of the language into which you could translate this Gospel literature. Your assistance would be appreciated.

If you have found salvation in Christ, or have been otherwise blessed through our Gospel literature, please let us know. We would like to thank God with you, and remember you further in our prayers.

Nous vous invitons a nous contacter pour faire des arrangements concernant de nouvelles traductions de notre litterature, nous informant de la langue dans laquelle vous pouvez traduire cette litterature evangelique. Votre aide sera beaucoup appreciee.

Si vous avez trouve le salut en Christ ou si vous avez ete beni par notre litterature, nous vous prions de nous le faire savoir. Nous aimerions remercier Dieu avec vous et prier pour vous.

Nos vos convidamos a nos contactar, afim de fazer qualquer arranjo concernente a novas traducoes de nossa literatura em outras lfnguas. Vossa assistencia sera muito apreciavel.

Se tem encontrado a salvacao em Cristo, ou se tem sido abencoado por intermedio da nossa literatura evangelica, faca o favor de nos informar. Pois nos gostarfamos de agradecer a Deus juntamente convosco, e lembra-lo sempre em nossas oracoes.

For free Gospel literature, books and tracts in over 538 languages, write to:

Pour obtenir gratuitement de la litterature evangelique, des livres et des traites en plus de 538 langues, ecrivez a:

Para obter gratuftamente a literatura evangelica, livros e folhetos em mais de 538 lfnguas diferentes escreva para:

Copyright ANGP

www.angp-hb.co.za

info@angp.co.za

ALL NATIONS GOSPEL PUBLISHERS
P.O. Box 2191
PRETORIA
0001
R.S.A.

A Gospel Literature Mission financed by donations
Une Mission de litterature evangelique financee de dons
Missao de literatura Evanqelica financiada por donativos

(Reg. No. 1961/001798/08)

The “HEART OF MAN” books can be viewed and downloaded using the following link:

www.angp-hb.co.za